Nuru ya Kiswahili, Juzuu 4(1), Juni 2025:58-85
DOI: https://doi.org/10.58548/2024nuru41.5885

# Usawiri wa Ukizinda kwa Mawanda ya Mtu katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka *Rosa Mistika* na *Harusi*

**Arafa Jumanne**
**Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kikuu cha Dodoma**
arafa.jumanne@udom.ac.tz

## Ikisiri

Makala hii inajadili ukizinda wa Waswahili katika riwaya za *Rosa Mistika* (1971) na *Harusi* (1984). Kwa ujumla, dhana ya ukizinda hujadiliwa katika mielekeo mikuu mitatu: vitu vya asili, sanaa, na mtu. Kwa muktadha wa makala hii, tunaitambulisha mielekeo hii kama mawanda. Lengo la makala hii ni kujadili vipengele vinavyozingatiwa na jamii za Waswahili katika kuuthamini ukizinda kwa mawanda ya mtu. Unapotazamwa katika mawanda haya, ukizinda hurejelea hali anayokuwa nayo mwanamke ambaye hajawahi kukutana kimwili na mwanamume. Utafiti uliozaa makala hii uliongozwa na Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi. Data zilikusanywa kwa kutumia njia ya uchambuzi wa matini na usaili. Makala inabainisha kwamba ukizinda katika mawanda ya mtu katika jamii za Waswahili huangaliwa kupitia vipengele vinne. Navyo ni: kutambua umuhimu wa kizinda, kulinda kizinda, kutafuta kizinda, na kupima kizinda. Kwa kuwa ukizinda katika jamii za Waswahili huchukuliwa kama kitu chenye thamani, hususani katika kipengele cha maadili, makala inapendekeza kuwa tafiti zaidi zifanyike kuhusiana na masuala ya ukizinda wa Waswahili kupitia tanzu zingine za fasihi ya Kiswahili. Aidha, utafiti linganishi unaweza ukafanyika kutoka jamii za Waswahili na nyingine ili kuona tofauti ya chukulizi zilizopo katika jamii hizo kuhusiana na masuala ya ukizinda katika mawanda ya mtu.

**Dhana za Msingi**: ukizinda, mawanda, mtu, Waswahili

**Utangulizi**

BAKIZA (2010) linafafanua ukizinda kuwa ni hali ya mwanamke kuwa na ngozi nyembamba kwenye mlango wa utupu wake. Ngozi hiyo nyembamba huwa kwenye mlango wa utupu kabla msichana au mwanamke hajaingiliwa na mwanamume. Hivyo, huondolewa punde msichana anapoingiliwa na mwanamume kwa mara ya kwanza. Daly & Wilson (1978) wanabainisha kuwa kuna kizinda cha asili na kizinda unde. Kizinda cha asili ni kizinda ambacho msichana anazaliwa nacho. Hujulikana pia kama kizinda cha utotoni. Kizinda unde ni kizinda bandia ambacho wasichana au wanawake hukitengeneza kwa kutumia malighafi na nyenzo mbalimbali. Hujulikana pia kama kizinda cha kisasa. Dhana hii ya kizinda cha kisasa imeibuka kutokana na maendeleo ya teknolojia. Si shabaha ya makala hii kumakinikia kizinda unde. Makala inajielekeza kwenye kizinda cha asili.

Fasili ya BAKIZA (2010) kuhusu ukizinda ni mtazamo mmojawapo wa kuifasili dhana hii. Sanga (2018) anaifasili dhana hii ya ukizinda kwa mtazamo mwingine. Anaeleza kuwa ukizinda hurejelea hali ya upya katika vitu. Maelezo haya yanachukua mwelekeo wa jumla katika kuufasili ukizinda kuliko unaoelezwa na BAKIZA (2010) ambao unafungwa kwa mtu pekee.

Dhana ya ukizinda hutazamwa katika taaluma mbalimbali. Baadhi ya taaluma hizo ni Sosholojia, Sanaa, na Afya (Mhlongo, 2009; Cheryl, 2012). Kwa mujibu wa Sanga (2018), dhana hii hujadiliwa katika mielekeo mikuu mitatu. Nayo ni: mwelekeo wa vitu vya asili, sanaa, na mtu. Katika makala hii, mielekeo hii inajadiliwa kama mawanda.

Kwa mawanda ya vitu vya asili, ukizinda hutazamwa kama upya unaodhihirika katika vitu mbalimbali, aghalabu, vitu vya asili, kama vile vyakula na pombe za jadi (Sanga, 2020). Kuhusu mawanda ya kazi za sanaa, Sanga (2018) anaeleza kuwa ukizinda hutazamwa kama upya wa kiubunifu unaoibuliwa na wasanii mbalimbali na kudhihirika katika kazi zao. Kwa mawanda ya mtu, ukizinda humaanisha ubikira, yaani mwanamke ambaye hajawahi kukutana kimwili na mwanamume kabla ya ndoa (Mhlongo, 2009; Cheryl, 2012). Cheryl (2012) anasisitiza kuwa, katika uga wa Sosholojia, hali ya ukizinda huangaliwa kama kitu chenye thamani kwa mtu, hasa mwanamke.

Dhana ya ‘mtu’ inatumiwa katika makala hii kwa maana tofauti na dhana ya ‘binadamu’. Dhana ya binadamu, kietimolojia, inatokana na maneno ‘*bin Adamu*’ yanayomaanisha kiumbe yeyote aliyetokana na Nabii Adamu, yaani kiumbe wa mwanzo kuumbwa na Mwenyezi Mungu (Islamic Propagation Centre, 2007). Nabii huyo (Adamu) alipoletewa kiumbe wa pili, Eva au Hawa, walianza kuzaa watoto. Uzao huo unaendelea hadi sasa. Hivyo basi, kwa mujibu wa Islamic Propagation Centre (2007), binadamu ni kiumbe yeyote anayetokana na Adamu. Hivyo, msingi wa neno hili ni maumbile—yeyote anayetokana, na hivyo kufanana pia, na Adamu ni binadamu.

Fasili hiyo ya dhana ya binadamu ni kinyume na ya mtu. Kwa muktadha wa Kiafrika, msingi wa neno hili ni tabia na mwenendo wa binadamu katika kuamiliana na wenzake katika jamii (Chuachua, 2011). Wakikazia tofauti baina ya dhana za binadamu na mtu, Chuachua (2016) na Ponera (2024) wanaeleza kuwa muamala wa mtu na wanajamii wenzake huweza kumfanya awe ‘mtu-kweli’ au ‘si mtu’. Wanamaanisha kuwa binadamu

mwenye tabia na mwenendo unaokubalika na jamii husika ndiye ‘mtu’ au ‘mtu-kweli’. ‘Mtu’ au ‘mtu-kweli’ ni binadamu mwenye thamani ya kijamii. Kinyume chake huwa ‘si-mtu’, yaani binadamu asiye na thamani mbele ya jamii. Mawazo haya yanamaanisha kuwa si binadamu wote wanaweza kuwa ‘watu’ bali ‘watu’ wote ni binadamu (Ponera, 2024).

Ufafanuzi huo kuhusu tofauti kati ya binadamu na mtu unatilia nguvu fikra za kuuita ukizinda unaotazamwa kwa kujielekeza kwa kiumbe huyu anayetokana na Adamu kama ‘ukizinda kwa mawanda ya mtu’ badala ya ‘ukizinda kwa mawanda ya binadamu’. Hii ni kwa sababu ukizinda unashughulikiwa katika makala hii kama dhana inayofungamana na maadili—ambayo iko karibu sana na suala la tabia au mwenendo. Hivyo, kwa ujumla dhana ya ‘ukizinda kwa mawanda ya mtu’ hukusudia kutazama heshima na thamani ya ukizinda inayohusianishwa kwa kiumbe mwanadamu.

Cooper & Nylander (2010) wanaeleza kuwa ukizinda ni suala linalothaminiwa na tamaduni za takribani jamii zote duniani. Wanabainisha kuwa jamii kama vile za Misri, Bangladesh, India, Indonesia, Afrika Kusini, na Iran bado zinaunga mkono ukizinda kama thamani ambayo haipaswi kuharibiwa katika kipengele cha ndoa kama sehemu mojawapo ya utamaduni. Mtazamo wa jamii hizo ni kuwa ukizinda kwa mwanamke ni kiwakilishi cha desturi zao.

Akitoa mawazo yanayoendana na ya Cooper & Nylander (2010), Moler (1982) anaumulika ukizinda kwa mawanda ya mtu katika jamii za Waswahili. Jamii zinazorejelewa hapa ni za Waafrika wanaopatikana katika ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi, kuanzia Kaskazini karibu na Pembe

ya Afrika hadi Kusini katika nchi ya Msumbiji (Sengo, 2009). Vilevile, jamii hizi, kwa mujibu wa Mulokozi (2017) na Mlaga (2017), hupatikana katika maeneo ya Mrima katika nchi kama vile Kenya, Tanzania, Uganda, na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Moler (*ameshatajwa*) anasisitiza kuwa, katika jamii za Waswahili, ukizinda ni mojawapo ya tunu ambazo hupaswa kuthaminiwa kwa hali na mali.

Mawazo haya ya Waswahili kuhusu kuuthamini ukizinda yamekaa kiujumla sana. Kwanza, kama tulivyokwisha kueleza, ukizinda hutazamwa katika mawanda mbalimbali. Hivyo basi, dhana ya kuthamini ukizinda inakuwa ya jumla kwa sababu kuna maswali yanayoibuka. Mathalani, "Waswahili huthamini ukizinda wa mawanda yote kwa namna sawa?", "Tunu hiyo huthaminiwa zaidi katika mawanda yepi?" na "Kwa mawanda yoyote, thamani hiyo huzingatiwa kupitia vipengele vipi?" Maswali haya yalichochea wazo na hamu ya kuutafiti ukizinda katika jamii ya Waswahili.

Kwa kuwa masuala mbalimbali yanayoihusu jamii husawiriwa katika sanaa, ikiwamo riwaya (Mlaga, 2017), utafiti ulifanywa katika riwaya teule za Kiswahili. Vilevile, kwa kuwa ukizinda hutazamwa katika mawanda ya asili, sanaa, na mtu, ni vigumu katika makala hii kuushughulikia ukizinda kwa mawanda yote. Hivyo, makala inajielekeza katika mawanda ya mtu. Makala inajadili vipengele ambavyo Waswahili hujikita kwavyo katika kuzingatia thamani ya ukizinda kwa mawanda ya mtu kama vinavyosawiriwa katika riwaya teule.

**Mihtasari ya Riwaya Teule**

Sehemu hii inawasilisha mihtasari ya riwaya zilizotafitiwa ambazo zimesaidia kutoa data za msingi za makala hii. Riwaya hizo ni *Rosa Mistika* (1971) na *Harusi* (1984).

**Muhtasari wa riwaya ya *Rosa Mistika***

Riwaya ya *Rosa Mistika* imeandikwa na Euphrase Kezilahabi. Ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1971 na *East African Literature Bureau*. Kwa mujibu wa Ponera (2014), riwaya hii ni ya kwanza kuandikwa na Euphrase Kezilahabi. Data zinazotumika katika makala hii zimetolewa katika toleo la mwaka 1971. Riwaya imegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza inamuangazia mhusika mkuu, Rosa, tangu utoto wake hadi kumaliza shule ya sekondari huko Mwanza. Sehemu ya pili ya riwaya inasawiri misukosuko ya mhusika mkuu huyo hadi kuharibikiwa kulikosababisha kifo chake. Mwandishi ametumia wahusika wengine kama Regina, Zakaria, Flora, Honorata, Deogratiasi na Charles ambao wamemjenga mhusika mkuu, Rosa, na mapito yake.

Mandhari iliyotumika katika riwaya hii ni ya vijiji vya Kisiwa cha Ukerewe pamoja na miji ya Mwanza na Morogoro ambako mhusika mkuu wa riwaya hii alipata kuishi na kusoma. Mandhari ya kutoka vijijini kwenda mjini katika shule za bweni yaliathiri tabia na matendo ya wasichana. Hii ni kutokana na mwingiliano wa wasichana wa kutoka sehemu mbalimbali. Fani iliyotumika katika riwaya hii ni ya kawaida na inaeleweka vizuri kwa wasomaji. Matukio yamepangwa kimfululizo. Hivyo, kila tukio katika riwaya hii linalikamilisha lingine.

**Muhtasari wa riwaya ya *Harusi***

*Harusi* ni riwaya iliyoandikwa na Abdallah Saffari na kuchapishwa mwaka 1984 na *African Proper Education Network*, Dar es Salaam. Toleo linalotumika katika makala hii lilipigwa chapa mwaka 2017. Riwaya imegawanyika katika sehemu kumi zilizoandikwa kwa kutumia namba.

Sehemu ya kwanza na ya pili zinazungumzia safari nzima ya mapenzi kati ya Jane na Dakta Mustaffa. Sehemu ya tatu inamhusu baba yake Dakta Mustaffa na utajiri wake. Aidha, sehemu hii inafafanua safari ya Dakta Mustaffa kupeleka taarifa ya kuoa nyumbani kwao. Baada ya kuifikisha taarifa hiyo, anapingwa vikali kwa sababu ya kutaka kumwoa mwanamke ambaye alishazaa nje ya ndoa. Sehemu ya nne na tano zinafafanua msimamo wa Dakta Mustaffa kuendelea kutaka kumwoa mwanamke aliyemchagua mwenyewe. Sehemu ya sita inaeleza wazo la mdogo wa Dakta Mustaffa, Rahman, kutaka kuoa, ambapo anasisitizwa na wazazi wake kuwa hawataki aibu kama ya kaka yake, Mustaffa. Sehemu ya saba inaeleza jinsi wazazi wa Rahman ambao ni Alhaji Mwinyi Karimu na Bibi Mahija Taadabuni wanavyochukua jukumu la kumtafutia mtoto wao msichana mwenye kizinda ili aweze kumwoa. Sehemu ya nane mpaka kumi zinaeleza jinsi harusi ya Rahman na Shufaa, binti wa Mwinyi Sitakishari, ilivyofanyika.

Fani iliyotumika katika riwaya ya *Harusi* ni nyepesi na inayoeleweka kwa urahisi. Vitushi vyake vimejengwa katika namna ya kukamilishana. Mandhari iliyotumika katika riwaya hii ni Tanga. Vilevile, kuna mandhari ya Tabora, Ujerumani, na Visiwa vya Komoro.

## Kiunzi cha Nadharia

Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi iliongoza utafiti uliozaa makala hii. Pia, nadharia hii imeongoza uwasilishaji wa data na mjadala unaofanywa katika makala hii. Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi iliasisiwa na Hippolyte Adolphe Taine katika miaka ya 1880 (Coser, 1963; Swingerwood, 1975). Kimsingi, nadharia hii hujikita zaidi katika kuangalia ufungamano uliopo kati ya mtunzi na jamii yake. Hivyo, mtunzi huonekana kama kiwakilishi

cha maisha halisi yanayojitokeza katika jamii yake (Mushengyezi, 2003). Narizvi (1982) anaongeza kuwa nadharia hii huzingatia uhusiano baina ya kazi ya fasihi na jamii katika kuhakiki kipegele chochote kinachosawiriwa katika maisha halisi ya mwanadamu. Hii ni kusema kuwa mtunzi huwa kama kioo kinachoakisi yale yanayojitokeza katika jamii yake na kuyaweka katika maandishi kupitia ubunifu. Nadharia hii inaongozwa na misingi miwili. Mosi, fasihi haiwezi kutengwa na jamii ambamo imeibuka. Hii ina maana kuwa fasihi hutokana na yale yaliyopo katika jamii husika. Pili, kila jamii huwa na maadili yake ambayo hutofautiana na maadili ya jamii nyingine (Wiredu, 1992; Mong'eri, 2000). Hivyo, kusawiriwa kwa maadili hayo huwa sehemu ya utamaduni wa jamii husika. Katika makala hii, misingi yote miwili imetumika kwa sababu ndiyo inayoakisi vyema yale yanayojitokeza katika fasihi na yanavyobainika katika jamii za Waswahili.

**Methodolojia**

Utafiti uliozaa makala hii ulifanyika maktabani na uwandani. Data za msingi za utafiti huo uliofanywa kwa mkabala wa kitaamuli zilipatikana kwa kutumia njia ya uchambuzi wa matini na usaili. Kupitia njia ya uchambuzi wa matini, riwaya za *Rosa Mistika* na *Harusi* zilisomwa na kuchambuliwa. Riwaya hizi zilichaguliwa kutumika kwa sababu zina sifa ya kipekee ya kusawiri masuala ya ukizinda wa Waswahili. Aidha, kupitia njia ya usaili huria, wanajamii wanne wa Mkoa wa Dodoma walihojiwa ili kupata maarifa yao kuhusu masuala ya ukizinda kwa kadiri yanavyosawiriwa katika jamii zao. Maswali mbalimbali yaliandaliwa na kuulizwa kwa watafitiwa ili kupata maoni yao. Data zilizopatikana zilichambuliwa kwa mbinu ya usimbishaji wa maudhui. Uwasilishaji wake ulifanywa kitaamuli, huku ukiongozwa na Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi.

## Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inawasilisha vipengele vinavyozingatiwa na Waswahili katika kuuthamini ukizinda kwa mawanda ya mtu kama vinavyosawiriwa katika riwaya zilizotafitiwa. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa Waswahili huuthamini ukizinda kwa mawanda ya mtu kupitia vipengele vinne. Navyo ni: kutambua umuhimu wa kizinda, kulinda kizinda, kutafuta kizinda, na kupima kizinda.

### Kutambua umuhimu wa ukizinda

Katika jamii za Waswahili, msichana hulelewa na kukuzwa kwa kukipa umuhimu kizinda chake. Wazazi hueleza watoto wao kuhusu umuhimu wa kutunza kizinda hadi siku ya ndoa. Sengo (1992) anasisitiza kuwa, katika jamii ya Waswahili, kizinda ni kitu muhimu kwa sababu ni sehemu ya maadili ya mtu. Kutokana na umuhimu huo, baadhi ya mabinti hudanganya kuwa wana kizinda hata kama hawana ili waonekane bora katika jamii zao. Hii ni kwa sababu jamii za Waswahili hufuata maadili na utamaduni wao (Farsy, 1956; Sengo, 1992). Riwaya zilizotafitiwa zinathibitisha kuwa jamii za Waswahili zinatambua umuhimu wa ukizinda katika kumletea heshima mwanadamu, hivyo, kumfanya aonwe kama 'mtu' mbele ya jamii.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, mwandishi anamchora Rosa akimdanganya mchumba wake, Charles, kwamba ana kizinda. Mwandishi anasema: "Vumilia kidogo muda umekaribia. Ninakuomba usiharibu kabla ya muda. Charles–mimi ni bikira." (uk. 78). Dondoo hili linathibitisha kuwa Rosa hakutaka kufanya mapenzi na Charles kabla ya ndoa kwa kuhofia kugunduliwa kuwa hana kizinda, hivyo, kupoteza heshima na thamani yake mbele ya Charles. Akitia mkazo suala hili, Maitaria (2019) anasema kuwa, katika utamaduni wa Waswahili, suala la ukizinda lina maana na hadhi

kubwa; hivyo, hupewa kipaumbele katika ndoa zao. Jaribio la ulaghai wa Rosa kwa Charles kuhusu kutofanya mapenzi linatokana na desturi za Waswahili kuwa tendo la jimai (kujamiiana) hufanywa na watu wawapo katika ndoa. Hivyo, jaribio la Rosa linatiliwa mkazo na Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi kupitia msingi unaosema kuwa kazi ya fasihi hutakiwa kufuata maadili na utamaduni wa jamii husika.

Jambo hili la kutambua umuhimu wa kutunza kizinda kwa mtoto wa kike linaendelea kuthibitika katika riwaya ya *Harusi*. Katika riwaya hiyo, mwandishi anatufafanulia namna Mkaza Sitakishari alivyokuwa akimsisitiza mume wake kuhusiana na binti yao anayetaka kuolewa kuwa bado ana kizinda. Mama huyo alikuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha binti yake anaenda kwa mume wake akiwa na tunu hii muhimu ya ukizinda. Hii ni kwa sababu jamii za Waswahili hukipa umuhimu kizinda kwa binti anapotaka kuolewa. Mwandishi anaeleza:

> Mkaza Sitakishari aliinua macho kumwangalia mumewe, kwa sauti thabiti akamweleza, "Kwa hilo nakataa mume wangu. Nathubutu hata kumlia yamini mwanangu. Shufaa mtulivu mithili ya maji mtungini. Hana macho ya utosini kama vijana wa marika yake." Alimaliza kwa sauti ya fahari kidogo "Poa mume wangu. Tutacheza harusi hoihoi jina lako na langu yang'are na kutangaa mume wangu." (uk. 59).

Katika nukuu hii, mama yake Shufaa anamtoa wahaka mume wake kwa kumweleza kuwa binti yake, Shufaa, bado anacho kizinda ambacho ni mhimili wa kuwapa sifa na ufahari wazazi hao mbele ya jamii. Kwa ujumla, dondoo hili linaeleza namna ukizinda ulivyo na thamani na unavyopewa umbele katika jamii za Waswahili kiasi cha wazazi kutilia mkazo katika harusi za watoto wao. Sengo (2009) anaeleza kuwa hali hii hutokana na

Waswahili kuamini kuwa, mwanamke asipokuwa na kizinda, mwanaume hatapata mke bora. Hivyo basi, kweli hii inayodhihirika katika jamii za Waswahili kama sehemu ya maisha yao ya kila siku inayakinishwa na msingi wa Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi usemao kuwa kazi ya fasihi hutakiwa kufuata maadili na utamaduni ambamo kazi hiyo imeibuka.

Aidha, katika jamii za Waswahili ukizinda una umuhimu kwa mwanamume anayetaka kuoa. Hoja hii inatokana na wanaume nao kutamani kupata wake wenye kizinda. Riwaya ya *Rosa Mistika* inalithibitisha hili baada ya Charles kubaini kuwa Rosa hana kizinda; hivyo akakataa kumuoa. Mwandishi anasema:

> … Ha Rosa, kweli wewe ulikuwa bikira. Unafikiri baada ya kufahamu kwamba ulichezewa sana huko Morogoro, na baada yangu mimi ninaweza kuona bonde la ufa na kuliona sikio, unafikiri mimi mwenyewe naweza kukuoa. Ha dada yangu sahau. Haiwezekani hata kwa mzinga. Hata kama ukiwa wa bure (uk. 90).

Dondoo hili linaonesha jinsi ukizinda ulivyo na umuhimu kwa mtu, hasa kijana anayetaka kuoa. Jambo hili lilimfanya Charles akatae kumuoa Rosa kutokana na kukosa kizinda. Hii ni ithibati kwamba ukizinda unabeba nafasi kubwa kwa msichana katika kuamua hatima ya ndoa yake. Ndiyo maana Charles aliona Rosa hana umuhimu tena kwake na kumpa maneno makali yenye kudhihaki utu wake. Akishadidia kuhusu suala hili la umuhimu wa ukizinda, Ramadhani (2023)[1] anasema:

> Zamani zile msichana alipotaka kuolewa ilikuwa lazima awe na bikira. Wakati sisi tunakua, ubikira ulikuwa unachukuliwa kama kipimo cha heshima ya mtoto wa kike. Hivyo, zamani ulikuwa huwezi kwenda kwa mume kama huna bikira kutokana na umuhimu wake.

[1]Bi. Asia Ramadhani ni mwanajamii aliyesailiwa na mtafiti mnamo tarehe 18/05/2023 nyumbani kwake Dodoma.

Nukuu hii inaonesha namna ukizinda ulivyokuwa na umuhimu katika maisha ya binti ili aolewe. Kwa kufanya hivi, binti ambaye alikuwa na kizinda alikuwa na nafasi kubwa ya kuolewa kuliko ambaye hana kizinda katika jamii za Waswahili. Aidha, binti huyo alikuwa anapewa heshima kubwa na wazazi pamoja na jamii inayomzunguka kutokana na kizinda chake.

**Kulinda kizinda**

Baada ya kuzingatia kipengele cha kutambua, jamii ina kipengele kingine kinachoujenga ukizinda kwa mawanda ya mtu. Kipengele cha kulinda ukizinda hupewa nafasi kubwa katika jamii ya Waswahili. Farsy (1956), Sengo (1992) na Harrison (2008) wanasisitiza kuwa wazazi au walezi humwongoza msichana kupitia mafundisho na maonyo kuhusu kuhakikisha msichana anabakia na kizinda hadi siku ya kuolewa. Hii hutokana na kizinda kuwa sehemu ya maadili na utamaduni wao; hivyo, huchukuliwa kuwa kijenzi muhimu cha utu wa mtu katika jamii.

Riwaya teule zinathibitisha suala hili kwa kuonesha namna wazazi na walezi wanavyolinda vizinda vya mabinti zao. Hufanya hivyo kupitia kukemea matendo ya uzinzi baina ya mtoto wa kike na kiume. Wanahofia mtoto wa kike atapoteza ukizinda kabla ya ndoa, hivyo, kuharibu heshima yao mbele ya jamii.

Jambo hili linabainika katika riwaya ya *Rosa Mistika* kupitia baba yake Rosa, Mzee Zakaria, ambaye anamchunga na kumkataza Rosa kuchangamana na wavulana ili asije kufanya mapenzi kabla ya ndoa na kuharibu kizinda chake. Katika kutekeleza dhamira hiyo ya Mzee Zakaria, mwandishi anaonesha namna Stella, mdogo wake Rosa, anavyomshtaki

Rosa kwa baba yake kwa kuchangamana na wanaume. Tunaoneshwa kuwa Mzee Zakaria anakuwa mkali hadi kufikia hatua ya kumpiga Rosa. Mwandishi anaeleza:

> Kwa Zakaria, Stella ndiye alikuwa msemakweli, na alimpenda kwa sababu hii.
> “Baba, Baba,” Stella aliita.
> “Mm,” aliitikia.
> “Leeo! Leeo! Rosa ali-alipata barua; barua pamoja na shilingi ishirini. Ametuonyesha.”
> Zakaria alichafuka, Rosa aliitwa mara moja. Rosa alikuja hali shuka ikimteremka chini. Kabla hajasema lolote, alipigwa na kuanguka chini. Alikuwa sasa mikononi mwa baba yake.
> “Lete hiyo barua, barua iko wapi? Pamoja na shilingi ulizopewa. Unafikiri sisi hapa maskini.”
> Rosa alipigwa tena na tena, makofi yalikwenda mfululizo hadi damu ikamtoka puani na mdomoni. Alilia, “Baba nihurumie sitarudia tena, nimekoma.” Rosa alinyang’anywa shuka. Chupi ilimuokoa lakini matiti yalikuwa nje (uk. 6).
>
> Zakaria hakujali; alichukua fimbo na kuongozana na bintiye mpaka chumba cha watoto hali akinguruma.
> “Lazima unioneshe barua hiyo! Unataka kuniletea umalaya wa mama yako hapa!
> Rosa alikuwa na haya nyingi; alichukua mfuko wake wa madaftari, na katika daftari la jiografia alitoa barua hiyo pamoja na shilingi tano. Alimpa babake shilingi hizo; lakini ile barua aliikunjakunja na kuitupia mdomoni. Alijaribu kuitafuna lakini babake alimkaba koo. Rosa hakuitema. Zakaria alikaza mkono. Macho ya Rosa yalianza kuwa mekundu, ulimi ulimtoka na barua ilianguka chini. Ilikuwa na utelezi kama kuku aliyetapikwa na chatu. Zakaria aliiokota mara moja.
> “Sema nani amekupa barua hii!”
> Charles, “Rosa alitamka kwa shida (uk. 7).

Kulingana na utafiti wetu, ukali wa Mzee Zakaria kuhusu binti yake kuwa na uhusiano na mwanamume unahusiana na ulinzi wa kizinda cha Rosa. Mzee Zakaria alimpiga Rosa ili akome kupokea barua kutoka kwa Charles ambaye anamtaka kimapenzi. Namna hii ya kulinda kizinda cha msichana inadhihirika pia katika jamii nyingi za Waswahili. Hivyo, hali hii anayoionesha Mzee Zakaria—ya ukali na kutoa adhabu ya kipigo—inaendana na msingi wa Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi unaosema kuwa fasihi haiwezi kutengwa na mambo yajitokezayo katika jamii husika. Kulingana na utafiti wetu, adhabu ya kipigo ni hatua ya juu ya ulinzi wa kizinda, ikiifuatia hatua ya ukali.

Mbali na kipigo, tunamwona Mzee Zakaria akitumia lugha kali na yenye matusi kwa kumwambia "Unataka kuniletea umalaya wa mama yako hapa!" Kauli hii inayomtusi pia mama yake Rosa, Regina, inaakisi tabia ya wanaume wengi katika jamii za Waswahili kunasibisha mwenendo mbaya wa mtoto wa kike na tabia ya mzazi wa kike (Sengo, 1992). Hivyo, hali hii inayakinishwa vema na msingi wa Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi unaosema kuwa kazi ya kifasihi haiwezi kujitenga na jamii iliyoizaa kazi hiyo. Ijapokuwa tukio lililoleta zahama hiyo kwa Rosa lilikuwa katika ngazi ya ombi tu (la mapenzi) la Charles kwa Rosa, Mzee Zakaria anachupa hatua nyingi mbele kwa kumfananisha Rosa na msichana malaya. Malaya, kwa mujibu wa BAKIZA (2010), ni mtu mwenye uhusiano wa kimapenzi na watu wengi. Hivyo, utafiti ulibaini kuwa Mzee Zakaria ameitumia dhana hii ya umalaya ili kuweka mkazo katika katazo la Rosa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanaume. Zaidi, tulibaini kuwa fikra ya kumhusisha Regina, mama yake Rosa, na tabia mbaya ya Rosa inalenga kumkumbusha Regina

na kuweka msisitizo kuhusu umuhimu wa kumchunga Rosa dhidi ya vitendo vya mapenzi.

Katika kuonesha kuwa Mzee Zakaria amedhamiria kulinda kizinda cha bintiye, Rosa, hakuishia tu kumpiga; bali, huku akimkokota Rosa, alimfuata pia Charles—kijana aliyemwandikia Rosa barua ya ombi la mapenzi—nyumbani kwao. Mwandishi anaeleza:

> Zakaria alianza kusema kwa sauti kubwa:
> "Charles! Tangu leo ukome kutembea na binti yangu. Chukua vishilingi vyako (alimtupia shilingi tano). Unafikiri sisi masikini tusio na mikono!"
> Alimshika Rosa shingoni kwa ukosi wa gauni lake akamsukuma kuelekea nyumbani kwake. Rosa alipofika nyumbani alikuta Regina amekwishamchemshia maji ya kumkanda usoni, kunywa na kuondoa damu mdomoni na puani. Baada ya kuoshwa alikwenda kulala. Alilia karibia usiku kucha (uk. 8).

Dondoo hili linaonesha jinsi wazazi wanavyotakiwa kuwakuza mabinti wao katika malezi. Hii ni kutokana na kuwa vijana hao wa kike hudanganyika na fedha zinazosababisha wajiingize katika mapenzi kabla ya kufikia umri wa kuolewa. Lengo la Mzee Zakaria kumfuata kijana huyo ni kumkanya asimfuate binti yake kimapenzi ili asiharibu kizinda kabla ya ndoa. Charles aliyekuwa akimtaka Rosa kimapenzi alikuwa anamrubuni kwa fedha ili aweze kumpata. Baada ya kubaini suala hilo, Mzee Zakaria alichukia na kuwa mkali kwa kuona kuwa Charles anataka kumharibia binti yake. Ni wazi kuwa hakuna mzazi ambaye hufurahia anapobaini bintiye anarubuniwa na wanaume. Kitendo hiki za Mzee Zakaria kinaendana na msingi wa Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi unaosema kuwa fasihi haiwezi kutengwa na jamii ambamo imeibuka ndiyo maana riwaya hiyo imesawiri namna hiyo

ya kulinda ukizinda. Kwa ujumla, mzazi huyu anawakilisha wazazi ambao wanafanya jitihada za kulinda ukizinda wa mabinti zao.

Halikadhalika, katika kushadidia suala hili la kulinda ukizinda katika riwaya hiyo, mwandishi anamwonesha Mzee Zakaria akiwafukuza vijana waliokuwa wanamtaka Rosa kimapenzi kwa kujifanya kuja kununua mayai nyumbani kwake. Anaeleza:

> …Walikuwa vijana wawili. Mmoja alikuwa na kofia kichwani. Rosa hakuwafahamu.
> "Shikamoo mzee" Zakaria hakusikia.
> "Mzee, shikamoo! Tunakusabahi," walipandisha sauti. Zakaria aligeuka nyuma kutazama ni akina nani.
> "Marahaba. Karibuni." Alijibu kwa upole. Aliendelea na kazi yake.
> "Rosa waletee viti wakae," Regina alisema.
> Rosa alileta viti viwili. Wale vijana walikaa wakitazama upande wa Rosa.
> Walikuwa bado wakifikiria namna ya kuanza kuzungumza Zakaria alipogeuka tena na kuwauliza kwa upole.
> "Mnataka nini watoto wangu?"
> "Mzee sisi tunatafuta mayai ya kununua."
> "Ooo kumbe mnatafuta mayai tu. Ninayo machache. Ninaweza kuwaleteeni lakini bei ni senti kumi kila yai; siyo senti tano."
> "Lete tu mzee, lete."
> Zakaria aliingia ndani ya nyumba. Vijana walibaki nje wakitabasamu.
> Alitoka na mayai matatu mfukoni. Walikuwa wakiyapima yale mayai kwa kuelekeza juani hali jicho moja wamefumba waliposhtukia viboko vinalia juu ya miili yao.
> "Mnafikiri mimi ni mjinga! Ondokeni hapa!" Wale vijana walikimbia bila kuangalia nyuma. Walifikiri bado anawafuata. Zakaria aliwasikia kwa mbali wakimtukana.
> "Mshenzi, utaoza na binti zako!" (uk. 23)

Kinachothibitika katika dondoo hili ni ukali wa Mzee Zakaria kwa binti yake, Rosa, katika kumlinda kimaadili ili asiharibikiwe katika maisha yake. Jamii za Waswahili zina seti yake ya maadili ambayo hutakiwa kufuatwa na kuzingatiwa na vijana hadi kufikia hatua ya ndoa. Hili linayakinishwa vyema na msingi wa pili wa Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi unaosema kuwa kazi ya fasihi ni lazima izingatie maadili maalumu ya jamii husika. Kusawiriwa kwa kitendo hicho kunathibitisha kuwa maadili hayo ni sehemu ya jamii za Waswahili. Suala hili la kulinda ukizinda linatiliwa mkazo na Hunde (2023)[2] anayesema:

> Kipindi chetu huko zamani wakati tunakua mtoto wa kike alikuwa akichungwa sana ili aweze kulinda bikira yake. Mtoto wa kike hakutakiwa kuchangamana kwa namna yoyote ile na mwanamume ili asiharibikiwe. Hivyo, ulikuwa ukionwa una ukaribu na mvulana yoyote ni lazima utakanywa kwa kutumia fimbo ili uache tabia hiyo.

Maelezo haya yanatufahamisha kuwa suala la kulinda kizinda cha mtoto wa kike katika jamii za Waswahili lilipewa kipaumbele ili kuhakikisha mtoto huyo anabakia nacho hadi wakati wa kuolewa. Kutokana na suala hilo, mtoto wa kike alichungwa sana na wazazi au walezi wake.

**Kutafuta kizinda**

Mbali na vipengele vya kutambua thamani ya kizinda na kulinda kizinda, jamii za Waswahili pia huuzingatia ukizinda katika mawanda ya mtu kupitia kipengele cha kusaka kizinda. Kipengele hiki cha kusaka kizinda huwahusisha wazazi/walezi pamoja na wanaume wanaokusudia kuoa. Ilibainika kuwa ni jambo la heshima katika jamii za Waswahili kwa wazazi na walezi kuwatafutia watoto wao wa kiume wasichana ambao ni bikira. Hii

[2] Bi. Milka Hunde ni mwanajamii ambaye alisailiwa na mtafiti mnamo tarehe 12/06/2023 nyumbani kwake Dodoma.

hutokana na mtazamo kuwa, katika muktadha wa ndoa, kizinda cha mwanamke huchukuliwa kama mali ya mume pekee (Kinsey, Pomeroy, Martin, & Gebhard, 1953). Mtazamo wa jamii za Waswahili ni kwamba mwanamume anatakiwa kuoa mwanamke ambaye hajaingiliwa, yaani bado ana kizinda cha tangu utotoni (Daly & Wilson, 1978). Hali hii, kwa mujibu wa Cooper & Nylander (2010) husababisha baadhi ya jamii kufanya uchunguzi ili kubaini kuwapo au kutokuwapo kwa kizinda kabla ya ndoa.

Kipengele hiki kimesawiriwa vema katika riwaya zilizotafitiwa. Katika riwaya ya *Harusi*, mwandishi anamsawiri Alhaji Karimu akiwa anaoa na kuacha wanawake kwa lengo la kutafuta mwanamke mwenye bikira. Mwandishi anaeleza:

> … Hivyo ndivyo ilivyokuwa milki ya Alhaji Karimu, aliyeoa na kutaliki wake zaidi ya mara kumi na mbili. Hatimaye aliridhika, au tuseme alichoshwa na tamaa ya bikira akabaki na Bibi Mahija Taadabuni binti wa Mwinyi mmoja kutoka Mkwaja, mwambao huohuo wa ushongo na Kipumbwi (uk. 23).

Dondoo hili linaonesha Alhaji Karimu alivyokuwa anawataliki wake zake kwa lengo la kupata mke mwenye kizinda. Kwa maana hiyo, kuhangaika kote huko kwa Alhaji Karimu kuoa na kuacha kunadhihirisha kuwa ukizinda una thamani pia kwa mume. Kwa upande mwingine, kitendo hicho cha kutafuta mwanamke mwenye kizinda kinaonesha kuwa, katika jamii za Waswahili, ukizinda ni tunu kubwa kwa msichana anapotaka kuolewa.

Mwandishi wa riwaya ya *Harusi* anatuonesha zaidi kuwa, mbali na mwanamume mwenyewe kusaka kizinda, wazazi pia hushiriki kuwatafutia watoto wao wa kiume watoto wa kike wenye kizinda. Kupitia baba yake Rahman, mwandishi anasema:

> Alhaji alimwangalia mke wake bila furaha sana akasema, “Basi vyema, pia siyo baya sana.” Halafu alimgeukia tena mke wake na kumweleza, “hili ni juu yenu sasa, wewe na wifi zako. Lakini tu nina akiba ya maneno; sitaki kipara moto wala guberi. Nataka mkaza mwana wa adabu na heshima, ashikaye dini *hamsa salawat*. Na sio jizee lililopigwapigwa huku na huku kama pia, alisema dhahiri akimkitia Jane … (uk. 55).

Vifungu vya “… sitaki kipara moto wala guberi …” na “sio jizee lililopigwapigwa huku na huku kama pia …” vinatuangazia mawazo na jitihada za wazazi kupendekeza na kusaka msichana mwenye kizinda ili aolewe na kijana wao wa kiume. ‘Kipara moto’ ni msimu unaorejelea mtu anayezini na watu wengi (BAKITA, 2017). Guberi, kwa mujibu wa TUKI (2004), humaanisha malaya. Zaidi, dhana ya ‘kupigwapigwa huku na huku kama pia’ inamanisha hali ya mwanamke kujamiiana na wanaume wengi.

Kinachosawiriwa katika dondoo hilo ni namna jamii za Waswahili zisivyopenda watoto wao kuoa wanawake ambao tayari walishaanza mapenzi na wanaume wengine. Wahusika wa kwenye dondoo hilo ni wazazi wa Rahman. Wanamtafutia mtoto wao mchumba bikira ili asilete aibu ya kuoa mwanamke ambaye tayari ameshafanya mapenzi kabla ya ndoa. Msomaji anaposoma dondoo hilo riwayani, inamfunukia akilini kuwa tahadhari hii inachukuliwa na wazazi wa Rahman kufuatia kaka yake Rahman, Mustaffa, kupeleka mwanamke ambaye alishazaa kabla ya ndoa. Wazazi huona kwamba jambo hili halifai katika mila zao, kwani linafedhehesha mbele ya jamii. Ili kujiweka mbali na ‘hatari’ hiyo iliyosababishwa na Mustaffa, wanaona bora wao wenyewe wamsake msichana atakayeolewa na Rahman. Zaidi ya sifa ya kuwa na kizinda, wanapendekeza msichana awe ametulia, ameshika dini, hajazaa, na mwenye

heshima. Akifafanua hoja hii ya kuhusu kutafuta ukizinda, hasa kwa mwanamume anayetaka kuoa, Mazengo (2023)[3] anasema:

> Hata sisi wanaume tunapenda mwanamke aliye na ukizinda. Kwanza huu ni ufahari kwa mwanamume kuwa amepata mke ambaye hajawahi kushiriki tendo la ndoa. Yaani, wewe ndio unaanza kumtumia. Wakati wetu kijana alipotaka kuoa wazazi/walezi au hata yeye mwenyewe alihangaika kwa hali na mali ili apate binti mwenye ukizinda. Familia ya binti aliyetaka kuolewa ilichunguzwa ili kuona kama binti huyo anafaa.

Nukuu hii inathibitisha namna ukizinda unavyotafutwa ili kukamilisha shughuli nzima ya harusi. Jamii za Waswahili zinaamini kuwa mwanamke mwenye kizinda huweza kuvumilia kutofanya mapenzi nje ya ndoa yake, tofauti na aliyefanya mapenzi kabla ya ndoa. Wakiyakinisha hoja hii, Kinsey & wenzake (1953), wanasema kuwa hali hiyo husababishwa na mwanamke huyo kutowahi kupata ladha ya mwanamume mwingine, tofauti na mume wake ambaye ametoa kizinda chake. Hivyo, huonekana kuwa na uwezo wa kutulia katika ndoa yake hata kama atakutana na ugumu wa maisha.

Zaidi ya hayo, imebainika kuwa katika jamii za Waswahili, iwapo kijana ataamua kulazimisha kuoa mwanamke ambaye familia haimtaki—yamkini, mwanamke ambaye hana sifa ya kuwa na kizinda—wazazi au walezi huamua kususia harusi hiyo na kumkataa mtoto wao. Suala hili hufanyika kwa lengo la kuleta heshima katika familia na jamii kwa jumla. Katika riwaya ya *Harusi*, suala hili linafafanuliwa kupitia Dakta Mustaffa anapolazimisha kumwoa Jane ambaye familia haikumkubali kutokana na kuwa alishafanya mapenzi kabla ya ndoa na kuzaa mtoto. Mwandishi anaeleza:

---

[3] Bw. Festo Mazengo ni mwanajamii ambaye alisailiwa na mtafiti mnamo tarehe 22/06/2023 nyumbani kwake Dodoma.

> "Basi mimi nasema ya mkato. Nimechoka kunyewa na mkojo wangu mwenyewe. Mchelea mwana kulia, atalia yeye! Mimi nasema." Alipandisha sauti zaidi, "Kama mimi Mwana wa Karimu kwelikweli na kwamba mimba ya Mustaffa nimeitia mwenyewe, haya na aoe!" Hakuna aliyemwingilia, hivyo naye akaendelea zaidi. "Na nasema hadhiri hapa, tena basi kwa kinywa kikuu, kwamba taraa, nafa leo hii, hana ruhusa ya kuyagusa wala kuyasogelea maiti yangu. Wala asiguse hata senti yangu moja au kuangua japo dafu moja tu kutoka viungani mwangu." Alimgeukia Mwanamimi na mkewe akawaambia kwa msisitizo, "Na nyiye nawaambia," aliinua kidole cha shahada cha mkono wa kulia akawa anakitingishatingisha mbele yao, "Si ruhusa kwa yeyote yule wa damu yangu kuhudhuria hiyo zinaa yao." Alimtazama zaidi mkewe kama asiyemuamini, akamwambia, "Na weye mwenye mwana ukenda huko nenda, lakini usitie tena mguu wako hapa." Alikielekeza kidole chake cha shahada chini kwenye sakafu ya pale sebuleni, *Wallahi* naapa Mungu mmoja (kur. 44 – 45).

Mustaffa alikumbwa na onyo hili analolitangaza bayana Alhaji Karimu, baba yake Mustaffa, kwa familia yake kutoitambua ndoa yake aliyoifunga. Hii ilitokana kwa kukiuka matakwa ya wazazi hao. Mbali na adhabu ya kutotambuliwa kwa ndoa yake, pia baba yake hakutaka kumwona mtoto wake katika maisha yake yote hata siku ya msiba wake.

Suala hili la wazazi au walezi kumtafuta msichana mwenye sifa, ikiwamo kuwa na kizinda, ili aolewe na kijana wao wa kiume linadhihirika katika jamii mbalimbali za Waswahili. Ni sehemu ya desturi walizojiwekea tangu enzi. Ndiyo maana wazazi huwa makini katika suala la kuamua harusi za vijana wao ili kulinda mila na desturi hizo. Kutokana na desturi hiyo, wazazi wana uwezo wa kuamua harusi kufanyika au kutofanyika kutokana na mila zilizopo katika jamii yao. Msingi wa Nadharia ya Sosholojia ya

Fasihi unaosema kuwa fasihi haiwezi kutengwa na mambo yajitokezayo katika jamii husika unathibitishwa vema na usawiri wa hali hiyo katika riwaya zilizotafitiwa. Hii ni kusema kuwa waandishi wa riwaya hizo huathiriwa na yale yaliyomo katika jamii zao na kuyaweka katika maandishi ili kufikisha ujumbe waliokusudia kufikisha kwa jamii.

**Kupima kizinda**

Jamii za Waswahili pia huuzingatia ukizinda katika mawanda ya mtu kupitia kipengele cha kupima kizinda. Ilibainika kuwa kipengele hiki ni sehemu ya desturi za Waswahili. Jamii za Waswahili hutoa kipaumbele katika jambo hili la kupima kizinda. Kitendo hicho cha upimaji kinaukilia ukweli kuwa familia nyingi katika jamii za Waswahili hufurahi na kujivunia watoto wao wa kike kukutwa na bikira kabla ya ndoa (Farsy, 1956). Hii ni kwa sababu hali hiyo huashiria kuwa familia hiyo imemlea binti yao katika maadili mema.

Mwandishi wa riwaya ya *Harusi* anasawiri kipengele hiki kupitia baba yake Shufaa, binti anayetakiwa kuolewa na Rahman. Anasema:

> "*Bismillahi*. Haya muungwana, kunani tena!"
> "Habi Sheulila (tulia)," Mwinyi Sitakishari alimtania. Kwa mas'hara alikuwa hapitwi na hawezekani. Mkewe alipopata pa kuketi pale juu ya kochi sebuleni ndipo aliendelea kumwelezea, "Nimekuita tuketi kikao nikuulize, upate nijibu." "Haya," alijibu huku akitumia upeto wa khanga yake kujipangusa jasho juu ya paji la uso wake. Mwinyi Sitakishari alimwangalia mkewe mboni za macho yake kwa muda hata mkewe akatia hofu kidogo.
> "Ni kuhusu huyo mwanao!" Mwinyi Sitakishari alianza kusema.
> "Nani, Shufaa!" Mwinyi Sitakishari aliitikia kwa kichwa akaendelea, "Nasema ya kuwa binti huyu kaposwa na ukoo wa watu na kwao, watu wenye kujinadi… kwani

> nani asiyemjua Alhaji Karimu. Maarufu Bara na Pwani. Umati utakaokuwepo siku hiyo utakuwa sio wa akina tonge domoni.
> … Alimkazia tena macho mke wake kwa nguvu zaidi, akaendelea, “Mimi nakwambia mke wangu sitaki fedheha! Yawa mwana wetu sio mzima bora turejeshe fedha za watu mara elfu! Upo hapo? ... Basi kama upo ndivyo vyema. Nipashe yanitue. Sema mwana mzima au keshamong’onyolewa?” (uk. 58).

Dondoo hili linaonesha jinsi wazazi na walezi katika familia za Waswahili wanavyokuwa na hofu ya aibu kutoka kwa watoto wao juu ya kuwapo au kutokuwapo kwa ukizinda kabla ya ndoa. Ili kujiweka mbali na aibu hiyo, huweza kumpima kwa njia mbalimbali ili wapate ukweli wa kuwapo au kutokuwapo kwa kizinda kabla ya ndoa. Topan (1995) anabainisha kuwa upimaji huo hufanywa kwa njia ya kudadisi na kufanya uchunguzi wa kijadi. Uchunguzi huo hufanywa na mzazi, mlezi au wakati mwingine hushirikisha jopo linalojumuisha jamaa wa karibu wa msichana anayepimwa, kama vile ndugu wa karibu wa baba yake na wale wa mama yake, yaani shangazi, bibi, mama mkubwa au mama mdogo. Watu hawa huaminiwa kuwa na tajiriba pana ya kutambua kuhusu kuwapo au kutokuwapo kwa kizinda kwa njia kama vile ya kutazama (Farsy, 1956).

Mwandishi wa riwaya ya *Harusi* anahitimisha mjadala wa upimaji wa kizinda cha Shufaa kupitia jibu la mamake Shufaa. Anasema:

> Kwa sauti thabiti, akamweleza, “Kwa hilo nakataa mume wangu. Nathubutu hata kumlia yamini mwanangu. Shufaa mtulivu mithili ya maji mtungini. Hana macho ya utosini kama vijana wa marika yake.” Alimaliza kwa sauti ya fahari kidogo “Poa mume wangu. Tutacheza harusi hoihoi jina lako na langu yang’are na kutangaa mume wangu.” (uk. 59).

Mwandishi anaonesha namna Mama wa Shufaa alivyo na uhakika na binti yake, Shufaa, kuwa na kizinda. Jibu hili ni matokeo ya uchunguzi alioufanya mama kwa bintiye. Katika jamii za Waswahili, uchunguzi huu hufanyika kutokana na wazazi au walezi kuogopa aibu ya binti yao kutokutwa na kizinda katika siku ya ndoa. Hivyo, binti alikuwa akidadisiwa au hata wakati mwingine kufanya tendo la kupima ukizinda ili ijulikane kama bado anao au hana. Thomas (2023)[4] anajazia hoja hii kwa kusema:

> Wazazi wa kike au mashangazi ndio walipewa jukumu la kuratibu masuala haya ya kuangalia kama binti ana ukizinda au hana. Wakati mwinge, wanaweza wasipime ukizinda lakini wakamuuliza kwa kumdadisi binti kama alishawahi kufanya mapenzi kabla ya kuolewa. Wakiamua kufanya kitendo cha kupima watachukua mashuka meupe na kutandika. Baada ya hapo binti na mchumba wake watalala damu ikitoka basi binti ana ukizinda. Kinyume na hapo, huwa aibu; na wakati mwingine binti hupewa adhabu ya kuzomewa.

Maoni haya yanatilia nguvu hoja ya upimaji wa ukizinda kabla ya siku ya ndoa ili kuepuka aibu kwa binti na kwa familia kwa ujumla. Middleton (1992) na Sanga (2018 & 2021) wanasema kuwa kipengele hiki huzingatiwa kwa sababu uamuzi wa kufanyika au kutofanyika kwa sherehe za harusi hutegemea majibu ya upimaji huo. Ikiwa kizinda cha mwanamke anayetaka kuolewa kitakutwa, sherehe ya harusi huendelea. Wazazi na bibi harusi hupewa zawadi kutokana na kukutwa kwa kizinda. Humaanisha wamefanya vema katika kumtunza mwari wao. Kinyume chake, sherehe ya harusi inaweza kuvunjika iwapo bibi harusi hatakutwa na kizinda. Kutokana na hili, nyimbo za fedheha na matusi huimbwa.

[4] Bi. Neema Thomas ni mwanajamii ambaye alisailiwa na mtafiti mnamo tarehe 14/07/2023 nyumbani kwake Dodoma.

**Hitimisho**

Makala hii imejadili namna riwaya za *Rosa Mistika* (1971) na *Harusi* (1984) zinavyosawiri ukizinda wa Waswahili kwa mawanda ya mtu. Makala imeweka bayana kuwa, kwa jamii za Waswahili, ukizinda katika mawanda ya mtu hukitwa sana katika kizinda cha asili, yaani kizinda cha tangu utotoni. Makala imeweka bayana kwamba ukizinda katika mawanda ya mtu katika jamii za Waswahili hutazamwa kupitia vipengele vinne. Navyo ni: kutambua umuhimu wa kizinda, kulinda kizinda, kutafuta kizinda, na kupima kizinda. Tafiti zaidi zinapendekezwa kufanyika kuhusiana na masuala ya ukizinda wa Waswahili kupitia tanzu zingine za fasihi ya Kiswahili. Aidha, utafiti linganishi unaweza ukafanyika kutoka jamii za Waswahili na nyingine ili kuona tofauti ya chukulizi zilizopo katika jamii hizo kuhusiana na masuala ya ukizinda katika mawanda ya mtu.

**Marejeleo**

BAKITA (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers.

BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

Cheryl, S. (2012). “The Guilt of Men” Re-visioning the Virgin Birth in Thando Mgqolozana's Hear Me Alone Current Writing: Text and Reception in Southern Africa, *Current Writing: Text and Reception in Southern Africa*, 24(2), 149-158. Inapatikana katika https:// doi.org/10.1080/101 3929X2012.706911.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert*. Dar es Salaam: TUKI.

Chuachua, R. (2016). *Falsafa ya Riwaya za Robert na Euphrase Kezilahabi katika Muktadha wa Epistemolojia ya Wabantu* (Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Cooper, R. & Nylander, L. (2010). *(de) constructing Sexuality and Virginity an Anthropological Analysis of Slidkrans in Sweden* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Sweden, Uppsala.

Coser, L. (1963). *Sociology through Literature*. New Jersey: Prentice-Hall.

Daly, M. & Wilson, M. (1978). Competitiveness, Risk Taking, and Violence: the Young Male Syndrome. *Ethology and Siciobiology*, 6(1), 1-78.

Farsy, M. (1956). *Ada za Harusi katika Unguja*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Harrison, M. (2008). "A Global Perspective: Reframing the History of Health, Medicine, and Disease". *Bulletin of the History of Medicine*, *89*(4), 639-689. Inapatikana katika https://www.jstor.org/stable/26309101.

Islamic Propagation Centre (2007). *Elimu ya Dini ya Kiislamu - Madrasa na Shule za Msingi: Kitabu cha Saba*. Dar es Salaam: Islamic Propagation Centre.

Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Kinsey, A., Pomeroy, W., Martin, C., & Gebhard, P. (1953). *Sexual Behaviour in the Human Female*. Saunders Publisher: London.

Maitaria, J. (2019). Methali za Kiswahili kama Wenzo wa Kubainishia Falsafa ya Kiafrika Kuhusu Familia. Katika A.S. Ponera na Z.A. Badru, (Wah.). *Koja la Taaluma za Insia*: *Kwa Heshima ya Prof. Madumulla* (Kur. 435-456). Dar es Salaam: Karljamer Publishers Ltd.

Mhlongo, P. (2009). *Reasons for Undergoing Virginity Testing: A study of Young People in Rural KwaZulu-Natal, South Africa* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha South Africa, Pretoria.

Middleton, J. (1992). *The World of the Swahilian African Mercantile Civilization: New Heaven*. London: Yale University Press.

Moler, A. (1982). *Love, Marriage and the Family: Yesterday and Today*. New York: Alba House.

Mong'eri, O. (2000). *Utetezi wa Maadili katika Fasihi-Nathari ya Shaabaan Robert* (Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Mlaga, W. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.

Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Mushengyezi, A. (2003). *Twentieth Century Literary Theories*. Kampala: Mukono Publishing Company.

Narizvi, S. (1982). *The Sociology of Literature of Politics*. Edamund Burke.

Ponera, A.S. (2014). *Ufutuhi katika Riwaya ya Kiswahili: Ulinganisho wa riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi* (Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Ponera, A.S. (2024). Uchimuzi wa Epistemolojia ya Wabantu kuhusu Ontolojia ya Mtu katika Riwaya za Shaaban Robert. *Mulika*, 42(2), 197-216.

Saffari, A. (2017). *Harusi*. Dar es Salaam: African Proper Education Network.

Sanga, A. (2018). *Mkengeuko wa Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi Andishi za Kiswahili Kipindi cha Utandawazi: Mifano kutoka Magazeti ya Habari Leo, Nipashe na Mwananchi* (Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Sanga, A. (2020). Athari za Mkengeuko wa Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi za Kiswahili. *Kioo cha Lugha*, 18, 172-188.

Sanga, A. (2021). Thamani ya Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi Simulizi za Kiswahili. *Mulika*, 40(1), 108-125.

Sengo, T.S.Y. (1992). Utamaduni wa Kiswahili: Wilaya ya Kusini-Unguja. *Nordic Journal of African Studies*, 1, 53-79.

Sengo, T.S.Y. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: Alamin Education and Research Academy.

Swingerwood, A. (1975). *The Novel and Revolution*. London: The Maccmillan Press Ltd.

Topan, F. (1995). A Virgnity Celebration Ceremony among the Swahili of Mombasa. *African Languages and Culture*, 8(1), 87-107.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Wiredu, K. (1992). African Philosophical Traditional. *The Philosophical Forum*, 34, 1-3.